MAFUNDISHO

HALISI YA MSINGI

YA KRISTO

DAR-ES-SALAAM CHRISTIAN LEADERSHIP COLLEGE. (DCLC)

Askofu Sylvester Gamanywa

Toleo la kwanza 2006

HL00004-006

ISBN9987-04-X

Haki zote zimehifadhiwa

WAPO MISSION,
BCIC Mbezi Beach
P.O.BOX 6178,
DAR ES SALAAM.

Kimepigwa chapa na:
BUSINESS PRINTERS LIMITED

YALIYOMO.

UTANGULIZI

SOMO LA KWANZA

KUZITUBIA KAZI ZISIZO NA UHAI
A) TAFSIRI SAHIHI YA NENO TOBA:
I. Tafsiri halisi ya Kibiblia
II. Kanuni ya kupata msamaha wa kweli kutoka kwa Mungu.
B) KAZI ZISIZO NA UHAI:
I. Matendo ya Mwili,
II. Miungu mingine

SOMO LA PILI

IMANI KWA MUNGU:
A)TAFSIRI YA NENO IMANI:
I. Tafsiri halisi ya Kibiblia.
B) KUSUDI LA IMANI NDANI YETU
C) MASHUJAA WA IMANI KATIKA BIBLIA
D) IMANI NA MAISHA YA KILA SIKU

SOMO LA TATU

MAFUNDISHO YA MABATIZO
TAFSIRI YA MANENO NENO MABATIZO NA UBATIZO
I. Tafsiri halisi ya kibiblia.

AINA 8 ZA MABATIZO KATIKA BIBLIA:
1. Ubatizo wa Musa
2. Ubatizo wa Yohana.
3. Ubatizo wa kiyahudi.
4. Ubatizo wa Yesu Kristo.
5. Ubatizo wa wanafunzi wa Yesu.
A) MTU ANAYESTAHILI KUBATIZWA:
B) SABABU ZA LAZIMA ZA UBATIZO:
C) MAHALI PANAPOKUBALIKA KWA AJILI YA
D)JINSI UBATIZO UNAVYOPASWA KUFANYIKA:

6. Ubatizo katika mwili wa Kristo.
7. Ubatizo wa Roho Mtakatifu.
8. Ubatizo wa moto.

SOMO LA NNE

KUWEKEA MIKONO:
A) MADHUMUNI YA KUWEKEA MIKONO
B) WANAOSTAHILI KUWEKEWA MIKONO
C) ATHARI ZA KUWEKEWA MIKONO
D) AWAMU ZA KUWEKEWA MIKONO:

SOMO LA TANO

UFUFUO WA WAFU.
A) AWAMU MBALIMBALI ZA UFUFUO

SOMO LA SITA

HUKUMU YA MILELE.
A) Hukumu ya Dhambi.
B) Hukumu za duniani.
C) Hukumu ya watakatifu.
D) Hukumu ya mataifa.
E) Hukumu ya mwisho.

MAANA YA MAFUNZO YA KWANZA YA KRISTO

1. Mafunzo ya kwanza ya Kristo yanatokana na maneno ya Bwana Yesu Kristo Mwokozi wetu wakati akiwaaga wanafunzi wake baada ya kufufuka alipokutana nao kabla ya kupaa kurudi alikokuwa kwanza; katika kitabu cha Mathayo 28:20 “na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi…”
2. Ni mafunzo ya msingi kwa kila aaminiye ambayo yanafanya mtu wa Mungu awe amejengwa juu ya mwamba. Mafunzo yanayofanya mtu adumu katika wokovu bila hofu wala kutetereka kwa lolote.
3. Kila mkristo anayetaka kufika mbinguni kwa kumaanisha ni lazima ajengwe juu ya msingi huu na kama hakuwahi kuyapitia kwa mtiririko wa namna hii, ni muhimu akayapata na kukaa chini akafundishwa. Nje ya hapo, safari yake ya kwenda mbinguni inaweza kuwa ngumu hata kama anataka kufika huko kwa sababu hataweza kushinda majaribu.
4. Haya ni mafunzo yanayotakiwa kuwa msingi wa kila kusanyiko ama kanisa endapo viongozi wana nia ya kuwapeleka watu mbinguni na kama msingi huu utapuuzwa, hicho kinachojengwa kitakuwa siyo cha Kristo hata kama anatajwa humo watu watakuwa dhaifu kiimani kama Bwana Yesu alivyosema alipotoa mfano wa wajenzi wawili waliojenga nyumba zao, mmoja juu ya mwamba na mwingine juu ya mchanga (Mathayo 7:24-27).

Msingi halisi wa Yesu Kristo ambao ndiyo imani sahihi umejengwa katika mambo makuu sita ambayo yanatakiwa yawe muhimili ndani ya kila mwamini na kanisa kwa ujumla. Mambo hayo sita yameandikwa katika kitabu cha (Waebrania 6:1,2) ambayo ni;-

1. **Kuzitubia kazi zisizo na uhai**
2. **Kuwa na Imani kwa Mungu**
3. **Mafundisho ya mabatizo**
4. **Kuwekea mikono**
5. **Kufufuliwa wafu**
6. **Hukumu ya milele**

Bwana wetu Yesu Kristo alikaa na wanafunzi wake kwa zaidi ya miaka mitatu akiweka msingi wa Kanisa lake ili hatimaye iwe rahisi kwao kuitambua imani sahihi ama potofu zinazoibuka duniani, ambapo kila imani potofu utaikuta imepotoa maana halisi ya Yesu katika mafundisho hayo sita.

Watu wenye imani ya Yesu Kristo hutambuana kwa kuwa na mtazamo mmoja na ufahamu mmoja husiopingana katika maana na tafsili ndani ya mafundisho hayo sita. Kimsingi inapotokea mgongano wa mawazo katika mafudisho hayo hapo juu, kuna uwezekano mkubwa wa fundisho hilo kutokuwa sahihi. Mafunzo hayo yamefafanuliwa moja baada ya jingine kwa undani katika kijitabu hiki.

SOMO LA KWANZA

KUZITUBIA KAZI ZISIZO NA UHAI:

Kazi zisizo na uhai zimegawanyika katika mafungu yapatayo mawili ambayo ni;

1. **Matendo ya Mwili**
2. **Kuabudu miungu mingine**

- Kuzitubia kazi zisizo na uhai kunatokana na mtu kuishi kwa kuufuata mwili na kufanya matendo yanayolazimishwa na mwili au kuishi kwa kuifuata miungu mingine badla ya Mungu aliye Hai.
- Matendo ya mwili hutokana na tamaa ya kuuridhisha mwili ambapo kuabudu miungu mingine hutokana na upofu wa kiroho unaomfanya mtu kuabudu kwa kuhisi kuwa

anachofanya yumkini kikawa ni cha Mungu; iwe ni kwa kudanganywa ama kwa kutengeneza yeye mwenyewe.

- Wakati huo huo Mungu ameweka njia moja tu ya mtu kuwa na uhusiano naye nayo ni TOBA ambayo mtu hulazimika kuifanya kwa sababu ya makosa yake.
- Hapa mwanzoni ni muhimu kuchunguza undani na maana ya neno toba ili kujua kanuni za Mungu anazotumia kumsamehe mtu.

TAFSIRI HALISI YA NENO 'TOBA'.

Kuna aina kadha za asili ya neno 'toba' kutoka lugha za kibiblia zilizotumika wakati wa Manabii na Mitume:

KIEBRANIA

1. **Nacham:** kughairi, na kuhuzunika moyo. (Mw.6:6, Kut.13:17, Ayu.42:6, Yon.3:10). =kughairi= **kubadili nia, kuacha mpango au jambo lililokusudiwa kwanza.**
2. **Shuwb:** kugeuka nyuma (1.Fal.8:47, Ez.14:6)
3. **Nocham:** Kujuta.(Hos.13:14)

KIYUNANI

1. **Metanoeo:** kubadili mawazo au fikra ili upate kufanya yaliyo mema kiroho, Au kubadili mwelekeo au mazoea juu ya dhambi.(Luka.13:3).
3. **Metamelomai:** kujutia madhara yatokanayo na dhambi, Mt.27:3,2Kor.7:8).
3. **Metanoia:** Badiliko halisi katika akili na mwelekeo mzima juu ya chimbuko au kiini cha dhambi, na sio tu kuhofia madhara yake. (Mt.3:8,11; 9:13; Luk.24:47).

Tafsiri halisi ya KUZITUBIA kazi zisizo na uhai:-

Ni tabia ya mtu wa Mungu kuishi maisha ya kuanguka na kusimama kila wakati kwa kukosa msingi imara. Hivyo kujikuta akishindwa kuhimili majaribu yanayokuja ili

kumlazimisha atende dhambi na kulazimika kutubu kila mara, jambo ambalo linaweza kumfanya kuachwa, Yesu atakaporudi ghafla.

Mtu anaposema au kufikiri juu ya kutubu kutokana na msingi wa Biblia lazima azingatie kuwa na ***"uamuzi thabiti wa kubadili nia na mwelekeo mzima juu ya dhambi, ikiwa ni pamoja na kugeuka nyuma na kuipa dhambi kisogo, kwa kusudi la kupatana na Mungu".***

Biblia inafunua wazi kwamba katika kanuni za msingi ili mtu aweze kupata msamaha wa kweli, Mungu huangalia ndani ya moyo wa mhusika endapo "***amefanya UAMUZI THABITI na WA HIARI wa KUBADILI NIA na mwelekeo mzima JUU YA DHAMBI, ikiwa ni pamoja na KUIJUTIA, na pia KUICHUKIA, na kisha KUIUNGAMA, na KUIPA KISOGO maisha yako yote".***

Kama umefuatana na mtiririko wa fundisho hapo juu kuhusu kuzitumbia kazi zisizo na uhai ambazo ni Matendo ya Mwili na kuabudu miungu mingine, basi sasa fuatilia uchambuzi wa kina juu ya mambo hayo.

MATENDO YA MWILI

Yanapatikana kwa wingi katika Gal 5:19-21; Mk 7:21-22; Rum 1:24-32; I Kor 6:9-11; Kol 3:5-10)

MIUNGU MINGINE

Kumb 5:6-10; Law 18:24-25; I Kor 10:14; 19-22; Kol 3:5-6; Mdo 15:29)

Kutokana na maandiko yaliyoorodheshwa hapo juu na mengine katika Biblia, miungu mingine imegawanyika katika makundi yapatayo matatu ambayo ni **"SANAMU ZA KAWAIDA** *(sanamu za kuchonga na vitu halisi kama mwezi, jua, miti, mawe", n.k).* ; Kuabudu **MASHETANI**

(mizimu ya mababu, ushirikina, kutegemea waganga wa jadi nk). Na ibada za **MAIGIZO YA AGANO LA KALE na za KUJITUNGIA.**

1. KUABUDU SANAMU ZA KAWAIDA:

Mungu aliwaonya vikali wana wa Israeli kuwa watakapokuwa wameingia katika ile nchi ya Ahadi, wahakikishe **wanawafukuza wenyeji wote wa hiyo nchi**, na **kuyaharibu mawe ya sanamu**, na **sanamu zao zote**, na **kubomoa mahali pao palipoinuka**. (Hes.33:50-56)

Pamoja na ushahidi wa kutosha kwenye maandiko matakatifu, bado hadi hivi leo tatizo la kuabudu sanamu linaendelea, na hata miongoni mwa wale wajiitao wakristo kwa majina ya dini.

Lakini haikuwa hivi wakati wa kanisa la kwanza. Historia inatuonyesha kwamba tangu miaka ya 100-400 A.D. ibada za sanamu na vinyago vilipigwa marufuku na kukemewa vikali na mitume wa kwanza.

Watu wa kwanza kuingiza mawazo ya kutengeneza sanamu na picha za mitume wa kwanza, na picha ya Yesu ni Ambrose na Augustine, ambao waliingiza hisia za kudhani kwamba picha na sanamu ni vielelezo kamili vya wahusika

Mwaka 784, Tarasius ambaye alikuwa mtetezi mkuu wa ibada za sanamu alichaguliwa kuwa Askofu Mkuu wa Mashariki. Mwaka 787, Sinodi ya Nikea ilihalalisha rasmi kuwa picha na vinyago viingizwe rasmi katika ibada na kuheshimiwa kama sehemu ya ibada. Uamuzi wa aina hiyohiyo ulifikiwa na kuidhinishwa kwenye sinodi ya Frankfort, huko Magharibi mwaka 794. Jambo hili lilikubalika tena huko Paris mwaka 825.

Kuanzia mwaka 850 A.D. ibada za sanamu zilipata umaarufu katika makanisa mengi ya wakati huo. Hii ilizidishwa zaidi na miujiza fulani iliyokuwa ikifanyika kupitia ibada za sanamu hizo. Hatimaye tena mwaka 1188 A.D. azimio jipya lilipitishwa kwamba kutokuabudu sanamu ni sawa na kumkana Mungu mwenyewe!

Mwaka 1225A.D. lilipitishwa azimio jingine jipya kwamba kama Kristo hatahifadhiwa kwa njia ya kumchora katika picha na sanamu hawezi kuwa Kristo kamili kwa wale wanaomwamini. Baadaye Thomas Aquinas alitangaza kwamba sanamu ya Yesu Kristo inachukua heshima ileile ambayo anastahili kupewa Yesu mwenyewe!

Kwa maelezo hayo hapo juu inaonesha wazi kwamba suala la kuabudu sanamu liliingizwa pasipo kufuata maongozi ya Roho Mtakatifu bali ni watu waliokengeuka walioingiza mawazo ya kuabudu sanamu kinyume na maelekezo ya Yesu pamoja na wanafunzi wake ambao mpaka wanaondoka duniani hawakuwahi kuingiza mawazo ya sanamu katika kanisa,

2. KUABUDU MASHETANI:

Lawi17:7; Kum 32:17; 2Nya 11:15; IKor 12:2; 1Kor 10:19-21; Law 19:28; Kum 14:1; Mdo 15:20

Ibada za mashetani ni pana sana kutegemea na mazingira na tamaduni za maeneo. Hizi zilizoorodheshwa hapa chini ni chache na zimetokana na mazingira ya Tanzania tu lakini tunajua kuwa kuna maeneo mengi yanayofanana ulimwenguni na baadhi yake ni, **“matambiko, kupiga ramli, kuangalia nyota, kupiga bao, kuwaomba na kuongea na wafu, kuwaombea au kuwaomba watakatifu waliolala mauti, kupunga majini, ngoma za ibada za kimila, kucheza au kusikiliza miziki ya wanamuziki wa kidunia, kutazama picha na filamu zote zinazohusiana na mambo**

ya zinaa, mazingaombwe, Kuabudu wanyama hai kama panya, ng'ombe, tembo n.k.).

3. IBADA ZILIZOPITWA NA WAKATI na za KUJITUNGIA (Yoh 4:19-24; Gal 4: 8-10; Kol 2: 16-17)

Ibada zote zilizokuwa zikifanyika kwenye Hekalu kabla ya Kristo kufa msalabani zote zilibatilika kwa kifo cha Yesu Kristo. Kifo cha Yesu kilisababisha pazia la Hekalu kupasuka toka juu hadi chini, kuonyesha kwamba aliyelichana ni Mungu na siyo mwanadamu, na kwamba huo ndio ulikuwa mwisho wa kutoa dhabihu na sadaka hekaluni.

Wakristo na madhehebu yote yanayojaribu kuigiza ibada mfano wa Agano la Kale na mavazi ya kikuhani, wanafanya ibada zilizopitwa na wakati.(Matt 27:51; Ebr 9:8-10; 10:9-10)

Lakini wakati huohuo kuna ibada za kujitungia wenyewe ambazo zimetokana na wanadamu katika jitihada za kumtafuta Mungu lakini kwa kuwa hazitokani na Mungu Mwenyewe, haziwasaidii kuushinda ulimwengu na mwili unakuwa na nguvu ya tamaa zinazowakosesha wanadam (

SOMO LA PILI

IMANI KWA MUNGU:

TAFSIRI YA NENO 'IMANI':

1. **'Pistis'** imani au kuamini, ni **'mahusiano** yaliyojengwa baina ya wahusika juu ya **msingi wa maagano maalum** yenye **uhusiano wa karibu,** na kwamba mahusiano hayo yanaendelea **kuboreshwa** na msingi huo huo.'

2. Neno hili lilitumika zaidi kwenye mikataba baina ya watu wanaofanya shughuli kwa ushirikiano. Kwa tafsiri hii, neno hili **'Pistis"** linadhihirisha tabia ya **uaminifu**juu ya **mkataba** uliopo baina ya wahusika.

3. Katika mtizamo huu, neno **'Pistis'** au 'imani', liliandikwa likimlenga Yesu Kristo kuwa ndiye **chimbuko, mwanzilishi, mkamilifu** kwa habari za kuanzisha na kushika maagano na wale wanaoamua kumfuata.

Imani inatokana na itikio la binadamu kwa ahadi za Mungu:

1. Imani kwa Ibrahimu iliambatana na Ahadi ya mtoto na kuwa baba wa mataifa mengi duniani.

2. Wakati wa Torati palikuwepo Ahadi ya Baraka iliyotakiwa kutanguliwa na UTII.

3. Kwetu sisi, kuna Ahadi ya utakaso na kukubaliwa na Mungu kupitia Yesu Kristo. (Yoh.1:29; Matt.26:26-29, Heb.9:13-15).

4. Kwetu sisi IMANI huzaliwa mara tu tusikiapo INJILI ya KRISTO, na **KUWEKA TEGEMEO** letu ndani ya **YESU KRISTO** (Rum 10:17).

Kwa maana hiyo ni kwamba imani halisi inayoweza kung'oa milima ya matatizo hutoka kwa Mungu baada ya binadamu kuitikia wito wa wokovu ndani ya moyo wake. (Yud 1:3)

KUSUDI LA IMANI NDANI YETU

(EBR.11:1) Kwa mujibu wa kitabu cha Waebrania, Imani ni uhakika wa wokovu usiotetereka kabisa. Inathibitika kwamba mtu akiokoka na kuipata Imani timilifu, hawezi kurudi nyuma tena na badala yake anakuwa ni nguzo katika kanisa.

Matumizi ya neon "imani" yametokana na neon "**hupostasis"** lenye tafsiri ya kiingereza ya **"SUBSTANCE"** yaani **"kitu halisi".** Kwa hiyo imani siyo mawazo wala hewa tu bali ni kitu halisi kinachomwezesha mtu kusimama imara bila

kutetereka kabisa; angalia kwa makini maelezo yanayofafanua imani ndani ya mwamini;-

I) **<u>Support</u> (mhimili):** Means to carry all or part of the weight of something and keep from falling or failing sinking etc. **(**Kubeba uzito wa kitu, kuzuia hali ya kuanguka, kuzama, au kushindwa).

2) **<u>Ground work</u>: (**kazi ya msingi inayobeba maisha ya mtu)
3) **<u>Confidence</u> au <u>firm trust</u>** (tegemeo thabiti)

4) **<u>Subsistance</u>; <u>to be kept alive</u>: (**uwezo wa kuwa kuwa na uhai na uwezo wa kumudu maisha).

SURA YA IMANI HALISI

a) Imani halisi ni kukubaliana na kufanya kama maneno yote ya Mungu pasipo mashaka yoyote moyoni juu ya kile alichokisema. (Ebr 11:1).

b) Imani halisi ni ile wanayokabidhiwa watakatifu mara moja tu, nayo ni takatifu sana. Hivyo wanaoipokea ni lazima wawe ni watakatifu kwa sababu imani halisi uhimiza utakatifu. (Yud 1:20)
c) Kwa maelezo rahisi ni kwamba hakuna uhusiano wowote kati ya Imani Takatifu na maisha ya dhambi au si sahihi kusema kwamba mtu anaweza kuwa na imani kwa Mungu aliye hai halafu akatetea maisha ya dhambi.

Watu wengi hupata shida wakati wokovu unapowakuta katika mateso kwa namna moja ama nyingine, katika hali hiyo, hushindwa kutofautisha kati ya wokovu unaotokana na kifo cha Bwana Yesu kwa ajili ya kuokoa na uponywaji wa miili yao. Jambo hili ni jepesi sana, uanachotakiwa kufanya ni kuangalia maeneo yafuatayo, wakati wa kutafuta uponyaji;

1. Kutafuta mlango ulioachwa wazi kwa kumpa Ibilisi nafasi
2. Dhambi iliyofichwa (isiyotubiwa na kuachwa)

3. Mikataba ya giza ambayo haijavunjwa.
4. Mitindo ya dunia iliyobuniwa na Shetani ili kuwanasa watu wa Mungu.
5. Kupenda anasa za dunia hii.
6. Upungufu wa neno la Mungu na maombi.

Ni ukweli kwamba kuna magonjwa ambayo huletwa na maisha yenye upungufu wa imani kwa Mungu ambapo mtu akigeuka na kumwamini Mungu magonjwa hayo hutoweka mara moja kwa kufuata kanuni ifuatayo:-

1. Kuziba kila mlango ulioachwa wazi
a) Kutubu kila dhambi na kuiacha kabisa (Mith 28:13)
b) Kuvunja kila mkataba wa giza (2Kor 6:14-16)
c) Achana na mitindo ya kuzimu na anasa za dunia (Rum 12:1; 1Pet 4:2:-4; Yoh 2:15-17; Yak 4:4
d) Hakikisha unajaa Roho Mtakatifu, Neno la Mungu na maombi. (1Kor 3:16-17; Efe 6:13-18; Kol 3:16)
2. Kuishi sawa sawa na kusudi la Mungu katika maisha yako
a) Tafuta kwa bidii kujua kusudi la Mungu katika maisha yako
b) Jitoe 100% kulitumikia kusudi la Mungu.

3. Kutumia mamlaka ya Yesu Kristo kuyapinga matatizo sugu
a) Tumia Jina la Yesu kukemea kila wazo linalokukatisha tamaa ya kupona
b) Tumia muda mwingi kuimba nyimbo za ushindi wa Yesu Kristo kwako.
c) Puuza kwa nguvu zako zote maumivu unayoyasikia na kutafakari Ukuu na uwezo wa Yesu Kristo aliyepata mateso zaidi ya hayo.

Mikono ya kiroho ya kupokea ahadi za mungu

a) Asiyeamini hawezi kupokea kitu toka kwa Bwana – (Yak 1:5-8; Ebr 5:7-10; 11:6).
b) Aaminiye ipasavyo atapata kila akiombacho – (Mk 11:22-24).

Imani huzaa afya njema

a) Yesu aliahidi kutupatia uzima tele (Yohana 10:10)
b) Hata wazee wameahidiwa afya njema kwa imani (III Yoh 1:2)

Imani ni kinga dhidi ya maadui wasioonekana

a) Tunalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani (1Petro 1:5)

Imani ni ipawa cha kuwahudumia wengine

Mtu anaposimama katika imani sawasawa anapewa vipawa vya kuwahudumia wengine kama Bwana Yesu alivysema na kuthibitishwa na maandiko matakatifu. (Mk 16:17; Yak 5:17-18)

Mashujaa wa imani katika biblia

Kuna mashujaa wa imani wa aina mbili katika Biblia; (Waebrania 11:1 – 40)

1. Mashujaa waliotikisa Falme, mamlaka na kutenda mambo ya kutisha mpaka Mungu akatukuzwa, na

2. Mashujaa walioteswa vibaya kwa ajili ya kumwamini Yesu Kristo na kufa kwa ajili ya imani yao. (Waebrania 11:32-40)

Wote hao wamewekwa kuwa mashahidi kwa ajili yetu tunaoishi sasa (Waebrania 12:1)

SOMO LA TATU

MAFUNDISHO YA MABATIZO

Tafsiri ya neno "Mabatizo":

1. Watu wengi hufikiri kwamba Biblia inaposema kuhusu mabatizo huzungumzia ubatizo wa maji tu, lakini sivyo kwa sababu ndani ya Biblia kuna mabatizo kadhaa tangu enzi za Musa hadi hivi leo.

2. Mabatizo mengine yamekwishapita na mengine yako mbele yetu na kila aliyezaliwa na Mungu lazima ayapitie ambapo ubatizo wa maji ni sehemu ndogo tu ya mabatizo hayo. Hayo yameelezwa kwa ufasaha katika somo hili kulingana na Bwana wetu Yesu alivyosema.

Tafsiri ya neno Batiza katika Biblia:

Japokuwa tafsiri za Kiswahili sanifu na kiingereza zimetoa maana ya ubatizo, bado maana hizo haziendani na maelekezo halisi ya kibiblia. Tafsiri halisi ya neno batiza kwa kutumia lugha ya kwanza aliyoitumia Yesu wakati akiwaagiza wanafunzi wake ni kama ifuatavyo;

Kiyunani: Batiza ni **"Bapto"** au **"Baptizo"** likiwa na maana ya **To dip in…** (kuchovya ndani ya…**Lk 16:24**) au **To dip under…**(Kutoelea ama kuzamisha ndani ya… **Yoh. 13:26**).

Aina mbalimbali za mabatizo

Kuna aina 9 za mabatizo katika Biblia, ambapo mabatizo manne ya mwanzo yamekwishapita na mengine matano yanahusika kwa kila anayemwamini Yesu sasa. Katika uchambuzi unaofuata, utaelewa kwa undani kile mwamini anatakiwa kukielewa kama Bwana wetu Yesu Kristo alivyokusudia tuelewe.

1. Ubatizo wa Musa:

Ubatizo wa Musa uliwahusu wana wa Israeli wakati wa kutoka Misri kwenda Kanaani pale walipopita katikati ya bahari ya Shamu. **(1Korintho 10:1,2)** Ubatizo wao ulikuwa ni katika wingu na katika bahari.

2. Ubatizo wa Kiyahudi: (Matt 23:15)

Ubatizo wa Kiyahudi ulitokana na agizo la Mungu kupitia Musa kwamba mtu yeyote ambaye si Mwisrael endapo alitaka kufuata torati ya Musa, ilimlazimu kuogeshwa (kuzamishwa) katika maji ya mto ama kisima kilichokuwa

karibu na Hema la kukutania au Hekalu kama njia ya kumsafisha. Njia hii ilitumika pia kuwarudisha wana wa Israeli waliokengeuka na kuifuata miungu mingine ambayo ndiyo aliyotumia Yohana Mbatizaji. **(Matt 23:15).**

3. Ubatizo wa Yohana: (Matt 3: Mk 1: Lk 3: na Yoh 1)

Ubatizo wa Yohana ulikuwa wa TOBA ambapo ulibeba unabii juu ya mambo makuu matatu:-

- Kutangaza watu kuja kwa Kristo (Masihi) (Lk 7:29-30, Yoh 1:23)
- Kutangaza kuja kwa Roho Mtakatifu (Matt 3:11, Lk 3:16)
- Kutangaza kuja wokovu na hukumu (Matt 3:12, Lk 3:17)

Ubatizo wa Yesu Kristo: (Lk 3:21, Matt 3:15)

Ubatizo wa Yesu Kristo unajitegemea kwa sababu Yeye hakuwa na sababu ya kutubu kwa kuwa wote waliokuwa wakitubu walikuwa wakitubu kumwelekea yeye, bali alifanya hivyo kwa ajili ya kuweka msingi wa mambo makuu mawili yafuatayo:

1. Kutuonesha kwamba imetupasa sisi sote kutimiza haki zote (Matt 3:15).

2. Kuweka msingi kwa kila aaminiye kufanya kama yeye alivyofanya kama ilivyoandikwa …*jitieni nira yangu, mjifunze kwangu… (Matt 11:29).*

Ubatizo wa wanafunzi wa Yesu: Kristo (Matt 28:19)

- Ubatizo wa wanafunzi wa Yesu Kristo unatokana na agizo la Yesu Mwenyewe wakati akiwaaga wanafunzi baada ya kufufuka.

- Moja kati ya mambo ya msingi kwa kila anayemwamini Yesu, ni jukumu la kufanya kama Yesu anavyoagiza katika Neno lake; huko ndiko kumpenda Yesu (Yoh 14:23, 24).

· Yesu ndiye aliyewaagiza wanafunzi wake akisema “Nendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi ***Mkiwabatiza*** kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu”

Kutokana na tafsiri ya maneno **‘Baptizo’** au **‘Bapto’** yaliyotumiwa na Yesu mwenyewe, Biblia imeonesha wazi kwamba waaminio wote walibatizwa katika maji mengi (walizamishwa).

Mageuzi na uamuzi wa kubadilisha namna ya kubatiza ulitokea tangu mfalme Constantine wa Rumi alipoamua kuigeukia Injili ya Kristo pamoja na maafisa wengi wa serikali ambapo ***mawazo*** ya kuwawekea watu maji kidogo kama ishara ya kuamini kwao pamoja na mawazo kwamba hata kama mtu hajabadilika moyoni anaweza kubatizwa bila kujali mambo yake ya ndani. Tendo hilo la kubatiza kwa matarajio kwamba linaweza kumwondolea mtu dhambi, huo ndio uliokuwa mwanzo wa ***wazo*** la kuwabatiza watoto. *(kubatiza kwa matumaini)*

Kimsingi mtu anakuwa ***Mkristo*** anapokuwa na uhusiano wa kweli na Kristo baada ya kutubu dhambi zake na kukusudia kuziacha kabisa. Hivyo ili mtu abatizwe katika ubatizo sahihi utakaofanya mabadiliko ya ki-Mungu ndani yake, lazima tendo la ubatizo litanguliwe na kumpokea Yesu na kuamua kuokoka kwa kuipokea imani halisi.

Inasisitizwa kwa wazi kwamba pasipo toba ya kweli (kuacha dhambi) moyoni, ubatizo hauna maana yoyote kwa mtu anayebatizwa. Ni kama kuogeshwa tu ndani ya maji.

Ubatizo katika mwili wa Kristo:

Ubatizo katika mwili wa Kristo unafanyika pale mtu anapobatizwa katika maji baada ya kuokoka. Ni tendo linalomaanisha kwamba “tumezikwa pamoja naye… na kufufuka pamoja naye kwa njia ya ubatizo (Rum 6:3-8, Efeso 4:5, Kol 2:12, Gal 3:27).

Mtu yeyote anapotamka kwamba ameokoka, hii ina maana moja tu; kwamba mwili wa dhambi umekufa na hana mpango wa kutenda nyingine. Hivyo mwili uliokufa, sharti uzikwe haraka, la sivyo utaleta shida.

“Zingatia” Endapo mtu anaamua kukataa kubatizwa baada ya kumpokea Yesu kama Mwokozi wake, ni sawa na aliyekufa kukataa kuzikwa; tafsiri yake ni kukataa kuingizwa katika mwili wa Kristo na lolote linaweza kumpata mtu wa jinsi hiyo hata kama alimaanisha kuanza maisha yanayompendeza Mungu.

Sababu za kubatizwa baada ya kuokoka

- Ni agizo la Yesu Mwenyewe (Matt 28:19, Mk 16:16, Mdo 2:38)
- Ni kiapo cha hadharani (Rum 10:9 – 10)
- Mtu aliyekufa pamoja na Kristo lazima azikwe (Rum 6:2-4; 11)
- Ni tendo la imani juu ya kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo – (Pet 3:21)

Jinsi gani mwamini abatizwe

1. Mbatizaji na mbatizwaji wote huingia ndani ya maji
2. Mbatizaji aombe sala maalum kwa ajili ya tukio hilo.
3. Mbatizaji amzamishe mwamini huyo ndani ya maji mengi.
4. Mbatizaji atamke utatu wa Mungu – Baba, Mwana na Roho mtakatifu (Matt 28:19).

Ubatizo wa Roho Mtakatifu: (Math 3:11, Mk 1:8, Lk 3:16, Mdo 2:1-4, 10:45 – 47)

- Kutokana na unabii wa Yohana Mbatizaji unavyosema, ni Yesu Kristo peke yake anayewabatiza watu kwa Roho Mtakatifu.

- Kinachothibitisha kwamba mtu ameokoka (amekuwa na ushirika na Yesu) ni kujazwa Roho Mtakatifu kwa ishara ya kusema kwa lugha mpya. Ni kushuhudiwa na Mungu

mbele ya waaminio kwamba sasa mtu yule ana uhusiano na Mungu (Mk. 16:17).

Ubatizo wa mateso: (Mk 10:38-39)

Mtu aliyeokoka anaweza kupitia katika mateso kwa namna moja ama nyingine kitu ambacho ni cha kawaida kwa mtu anayekwenda Mbinguni. Kuna mateso ya aina nne tofauti ambayo yanaweza kutokea katika maisha ya mwamini:-

- Mateso ya kuchukiwa – (1Fal 22:8-28)
- Mateso ya kuishi maisha magumu - (1Fal 22:24-28)
- Mateso ya kudhihakiwa na kutengwa - (Matt 23:29-34)
- Mateso ya maumivu makali hata kufa – Ufu 2:10, Mdo 7:59 – 60)

Ubatizo wa moto: (Math 3:11-12, Lk 3:16-17)

Ubatizo wa moto unahusika na kumtengeneza mtu wa Mungu ili kumwezesha kuishi maisha safi yasiyolaumika. Kuna maeneo matano muhimu ya kuangalia:-

Endapo mtu aliyeokoka ana tabia zisizofaa na anashauriwa lakini hataki kubadilika, anaweza kupitia mambo magumu ambayo hakuyatarajia lakini lengo la Mungu likiwa ni kutengeneza tabia zake sugu, kwa kutengeneza maeneo yafuatayo, ili yawe kama Yeye anavyotaka;-

- Tabia ambazo zinaleta matatizo katika jamii ili tuweze kuzaa matunda na hatimaye tufanane na Kristo. (1Pet 4:12, Mith17:3, Mith 27:21)
- Tabia ya kutokujali inayosababisha mtu asiwe msaada kwa wengine hivyo kazi ya moto ni ili tuwe na chumvi ndani yetu; tutamanike katika jamii inayotuzunguka badala ya kuwa vikwazo. (Math 5:13; Lk 14:25-35)
- Tabia ya magomvi yasiyoisha miongoni mwetu na hivyo kumlazimu Bwana atupitishe mahali fulani ili tuweze kukaa kwa amani sisi kwa sisi (Mk 9:50)
- Njia iliyochaguliwa na Mungu na inayofaa kubadili tabia ya mtu ni kutiwa chumvi kwa njia ya moto, basi. Hakuna njia mbadala. (hapa panahitaji uvumilivu na kukubali

kutengenezwa kama mtu aliyeazimu kwenda mbinguni. (Mk 9:49; Matt 3:11)

· Mwenye kazi ya kutia chumvi ni Roho Mtakatifu (Rum 15:16)

SOMO LA NNE

KUWEKEA MIKONO

Kuwekea mikono kunatokana na maneno ya Bwana Yesu alipowaagiza wanafunzi wake kwamba “Mtaweka mikono yenu juu ya wagonjwa nao watapata afya” (Mk 16:18).

Tangu Agano la kwanza (kale) watu waliwekewa mikono kwa kusudi la kupata baraka kutoka kwa Mungu;

a) Wakati wa kubariki (Mw 48:14, Math 19:15)
b) Wakati wa kutengwa kwa ajili ya huduma maalum (Hes 8:10, 27:22-23, Mdo 13:1-3)
c) Wakati wa kupokea karama za Mungu (Kumb 34:9, 1Tim 4:14, 2Tim 1:6)
d) Wakati wa kupokea uponyaji (Lk 4:40, 13:13; Mk 16:18)

Anayestahili kuwekea watu mikono:

1. Wazazi kwa watoto wao (Isaka kwa Yakobo na Esau)
2. Mtumishi aliyekwisha wekewa mikono (Anania kwa Paulo)
3. Mtumishi mwaminifu katika imani (Musa kwa Yoshua)
4. Mtumishi mwenye upako maalum (Eliya kwa Elisha, Yehu) n.k

Athari za kuwekewa mikono isivyostahili

1. Kupokea roho isiyotoka kwa Mungu (Kisa cha Simoni mchawi Mdo 8:18-24)
2. Kupokea laana badala ya baraka (Mafarisayo Math 23:15)

SOMO LA TANO

KUFUFULIWA WAFU

Ufufuo wa kwanza:

1. Kufufuka ni moja kati ya mafundisho muhimu katika kumwamini Yesu Kristo kama yeye alivyosema (Yoh 5:21-29, 6:39,40,44)
2. Tumaini letu katika imani ni katika ufufuo wa wafu (1Kor 15:1-8, 20-58)
3. Ufufuo wa kwanza ndio wenye maana na matumaini (Ufu 20:6)

Manabii nao walitabiri kuhusu ufufuo:

· Ayubu wakati wa mateso yake alipata ufunuo juu ya ufufuo (Ayu 19:25-26)
· Nabii Isaya alitabiri kuhusu wafu kufufuka (Isaya 25:8; 26:19)
· Danieli naye alitabiri habari za kufufuka waliokufa (Dan 12:2)

Ufufuo wa pili:

· Watu wote watakusanyika mbele ya kiti cha enzi kikubwa cheupe (20:12)
· Ufufuo wa pili utawahusu waliokataa kutii Neno la Mungu na Manabii (Ufu 20:5)
· Wanadamu wote walioishi kinyume na mapenzi ya Mungu mahali popote pale ambapo mauti iliwakuta wakaondoka duniani bila kumcha Mungu, hiyo ndiyo siku ya wao kufufuka na kujikuta wako mbele ya kiti cha enzi (Ufu 20:13)

· Watakaofufuka wakati huo hawatakuwa na sehemu katika uzima wa milele bali kutupwa katika ziwa liwakalo moto na kiberiti (Ufu 20:15, 21:8)

SOMO LA SITA

HUKUMU YA MILELE

Hukumu ya milele ni moja kati ya mafundisho ya msingi na hapo ndipo penye kutazamiwa na wote wanaomwamini Yesu.

Pamoja na kuwepo Hukumu ya milele itakayofanyika mwishoni mwa mabo yote, Mungu katika uwezo wake ametoa mamlaka ya hukumu za hapa duniani.

Pamoja na kuwepo na mamlaka za serikali zinazotumia Sheria na mahakama; lakini kuna hukumu za aina tatu zihusikanazo na maisha ya kiroho tangu mtu anapookolewa akiwa hapa duniani.

1. Hukumu ndogo ndogo za duniani:

a) Bwana Yesu aliweka kanuni ya namna ya kutatua matatizo miongoni mwa wanafunzi wake Math 18:15-20, (Pia kutii mamlaka Serikali iliyopo madarakani Rum 13:1-5)

b) Hukumu hizi zimeachwa chini ya mamlaka ya Kanisa ili kuwafanya waliookoka kumaliza matatizo yao wenyewe badala ya kushitakiana katika vyombo vya kibinadamu kwa kuwafanya wasiomjua Mungu kuamua juu yao (1Kor 6:1-7; 5:1-5; 9-13)

2. Hukumu ya Watakatifu:

Hukumu kwa watakatifu ni jambo la muhimu alilolieleza Bwana Yesu nayo imegawanyika katika maeneo makuu mawili;-

I. Hukumu ya watakatifu wakati wakiwa hapa duniani;

i) Bwana Yesu ameweka njia ya kuwashughulikia wale ambao wanafanyika kuwa wana wa Mungu lakini hawafanyi mapenzi ya Mungu (1Kor 11:17-34)

a. Wengine wanaweza kupatwa na magonjwa yasiyotibika kwa sababu ya kutumia Neno la Mungu vibaya.

b. Wengine wanaweza kufa kabla ya wakati kwa sababu ya kutumia Neno la Mungu vibaya.

II) Hukumu ya watakatifu baada ya kunyakuliwa;

a) Hukumu ya Watakatifu itafanyika baada ya waliookoka kunyakuliwa na kukutana mbele ya Kiti cha Hukumu cha Kristo (2Kor 5:10)

b) Kila kazi ya mtu itapitishwa katika moto na kuijaribu ni ya namna gani kutegemeana na nia ya mtendaji na jinsi alivyotenda (1Kor 3:10-15)

3. Hukumu ya mwisho:

a) Hukumu ya milele ni uamuzi wa mwisho kabisa utakaotolewa na Mungu mwenyewe siku ya mwisho wakati Mungu atakapofunga kila kitu kuhusu binadamu.

b) Watakatifu wataanza maisha ya raha milele na milele katika mbingu mpya na nchi mpya ambamo hapana bahari (Ufu 21:1-7, 22:1-5)

c) Watenda maovu wataanza maisha ya mateso milele na milele (Ufu 20:10, 21:8)